TANGAZO LA SERIKALI NA. 635 la tarehe 28/10/2022

SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI,
(SURA YA 283)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 44(1))*

KANUNI ZA UWINDAJI WA KUJIKUMU WA WENYEJI ZA MWAKA 2022

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kifungu* *jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTENGAJI WA MAENEO, UTARATIBU WA MAOMBI NA
UTOAJI WA VIBALI VYA UWINDAJI WA WENYEJI

3. Utengaji wa maeneo ya uwindaji wa wenyeji.
4. Utangazaji na usimamizi wa maeneo ya uwindaji wa wenyeji.
5. Maombi na utoaji wa kitambulisho cha mwindaji mwenyeji.
6. Maombi ya Kibali cha uwindaji.
7. Utoaji wa vibali vya uwindaji wa wenyeji.
8. Masharti ya utoaji wa kibali cha uwindaji wa wenyeji.
9. Masharti ya nyongeza.
10. Kundi la wawindaji na wageni watazamaji.
11. Mgao wa wanyamapori.
12. Jamiii za jadi.
13. Urejeshaji wa kibali cha uwindaji wa Wenyeji.
14. Uuzaji wa nyamapori.
15. Mwindaji mwenyeji kubeba kitambulisho.
16. Kupotea kwa kitambulisho.

17. Usimamizi wa nyara.
18. Uhamishaji wa nyara.

SEHEMU YA TATU
MAKOSA NA ADHABU

19. Adhabu ya jumla.

SEHEMU YA NNE
MASUALA MENGINEYO

20. Miongozo.
21. Rufaa.
22. Kufuta.

MAJEDWALI

SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI,
(SURA YA 283)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 44(1))*

KANUNI ZA UWINDAJI WA KUJIKUMU WA WENYEJI ZA MWAKA 2022

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uwindaji wa Kujikimu wa Wenyeji za Mwaka 2022.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"kundi la wawindaji" maana yake ni mgeni mwindaji, mfuatilia nyayo za wanyama, mchunaji wa ngozi, dereva pamoja na vibarua;

"mgeni mtazamaji" maana yake ni mtu ambaye amemsindikiza katika uwindaji mgeni mwindaji wa kienyeji kwa ajili ya kushuhudia shughuli ya uwindaji;

"mkazi" maana yake ni mtu ambaye ni mkazi mwenyeji wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

" uwindaji wa kujikimu" maana yake ni uwindaji unaofanywa na wenyeji kwa ajili ya matumizi ya kujikimu;

"ada zilizoainishwa" maana yake ni ada za wanyamapori kama zilizoanishwa katika jedwali la Pili la kanuni;

Sura ya 283

"afisa aliyeidhinishwa" maana yake ni kama ile iliyotolewa katika Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori;

"maeneo yaliyotengwa" maana yake ni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wenyeji na shughuli za uwindaji wa kujikimu;

Sura ya 283

"nyama" maana yake ni kama ile iliyotolewa katika Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori;

Sura ya 283

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori;

## SEHEMU YA PILI
## UTENGAJI WA MAENEO, UTARATIBU WA MAOMBI NA UTOAJI WA VIBALI VYA UWINDAJI WA WENYEJI

Utengaji wa maeneo ya uwindaji wa wenyeji

3. Waziri anaweza kutenga maeneo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za uwindaji wa wenyeji.

Utangazaji na usimamizi wa maeneo ya uwindaji wa wenyeji

4.-(1) Kamishna Mhifadhi anatakiwa kutangaza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwindaji wa wenyeji.

(2) Kamishna Mhifadhi, kwa kushirikianana Halmashauri ya Wilaya husika, atasimamia shughuli za uwindaji wa wenyeji katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwindaji wa wenyeji.

Maombi na utoaji wa kitambulisho cha mwindaji mwenyeji

5.-(1) Kwa madhumuni ya kukidhi masharti ya utoaji wa kibali cha uwindaji kwa wenyeji, mtu ataomba kwa njia ya maandishi kwa Kamishna Mhifadhi kitambulisho cha mwindaji mwenyeji.

(2) Kamishna Mhifadhi anaweza kutoa kitambulisho kwa muombaji aliyefaulu mtihani kwa vitendo wa uwindaji wa wenyeji baada ya kulipa ada ya Kitambulisho cha Mwindaji Mwenyeji kama ilivyoanishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi.

Maombi ya Kibali cha uwindaji

6. Mtu yeyote ambaye anataka kufanya uwindaji wa wenyeji ataomba kibali cha uwindaji kwa Kamishna Mhifadhi kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Utoaji wa vibali vya uwindaji wa wenyeji

7.-(1) Kamishna Mhifadhi au afisa leseni atatoa kibali cha uwindaji wa wenyeji kwa madhumuni ya uwindaji wa kujikimu tu kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(2) Kibali cha uwindaji wa wenyeji kitatolewa kwa mwombaji aliyelipa gharama zote za uwindaji wa wenyeji kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili na Jedwali la Tano la Kanuni hizi.

(3) Kibali cha uwindaji wa wenyeji kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(4) Kibali cha uwindaji wa wenyeji kitakuwa halali kutumika ndani ya mipaka ya wilaya husika kwa masharti yaliyoainishwa ndani ya kibali.

Masharti ya utoaji wa kibali cha uwindaji wa wenyeji

TS. Na. 267 la mwaka 1974
Sura ya 283

8. Kamishna Mhifadhi au afisa leseni wakati wa utoaji wa kibali cha uwindaji wa wenyeji kwa mwombaji atahakikisha yafuatayo-

(a) Ana leseni halali ya umiliki wa silaha ya moto;
(b) ana silaha sahihi kwa shughuli za uwindaji kama inavyoainishwa na Amri ya Silaha Sahihi;
(c) hajawahi kukutwa na hatia ya jinai kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori;
(d) anakitambulisho cha mwindaji mwenyeji kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi.

Masharti ya nyongeza

9. Kila mmiliki wa kibali cha uwindaji wa wenyeji atazingatia masharti yafuatayo-

(a) atarudisha kibali kwa afisa anayetoa ndani ya kipindi cha siku thelathini baada ya muda wake kuisha au baada ya uwindaji uliofanikiwa;
(b) hakuna kibali kipya kitakachotolewa kabla ya urejeshaji wa kibali cha awali;
(c) atahakikisha anazingatia masharti ya kifungu cha 45(4) cha Sheria;
(d) kwa mwindaji asiye mkazi anatakiwa kubeba kibali cha makazi wakati wote wa uwindaji;
(e) atahakikisha anaondosha taka zote zinazoweza kuharibika na zisizoharibika kwa njia salama na rafiki kwa mazingira;
(f) aambatane na afisa aliyeidhinishwa; na
(g) atahakikisha kwamba anaripoti katika eneo la kuingia na kutoka kama ilivyoainishwa katika leseni kabla na baada ya uwindaji.

Kundi la wawindaji na wageni watazamaji

10.-(1) Mmiliki wa kibali cha uwindaji atakuwa na haki ya kuambatana na kundi la wawindaji wasiozidi watu nane.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), taarifa za kina za kundi la wawindaji zitawasilishwa kwa Kamishina Mhifadhi kama zinavyoanishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(3) Mgeni mtazamaji anayeambatana na mwindaji mwenyeji katika safari ya uwindaji anapaswa kuwa na umri wa miaka sita au zaidi.

(4) Kibali cha uwindaji kitaruhusu wageni watazamaji wasiozidi sita.

(5) Wageni watazamaji watatakiwa kulipa ada kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tano la Kanuni hizi.

Mgao wa wanyamapori

11.-(1) Kamishina Mhifadhi baada ya kupokea ushauri kutoka Kamati ya Mgao wa Uwindaji wa Wanyamapori iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria, ataweka mgao wa wanyamapori wa uwindaji wa wenyeji utakaotumika kwenye msimu husika katika maeneo tengwa.

(2) Mgao wa uwindaji wa wanyamapori kwa ajili ya wenyeji utapelekwa kwa Afisa Wanyamapori wa wilaya husika.

(3) Hakuna kibali cha uwindaji kitatolewa nje ya idadi ya wanyamapori waliotolewa kwa uwindaji wa wenyeji katika halmashauri husika.

Jamiii za jadi

12.-(1) Jamii za jadi zitaruhusiwa kuwinda katika maeneo yao asili na Kamishna Mhifadhi atasimamia na kudhibiti wanyamapori watakaowindwa.

(2) Kwa matumizi ya Kanuni hizi , "Jamii za Jadi" maana yake ni Wahadzabe wanaoishi katika Wilaya za Mbulu na Iramba na Wandorobo wanaoishi katika Wilaya za Simanjiro na Kiteto

Urejeshaji wa kibalicha uwindaji wa Wenyeji

13.-(1) Mmiliki wa kibalicha uwindaji wa wenyeji atarejesha nakala ya kibali husika kwa afisa leseni ndani ya siku 30 baada ya muda wake kuisha.

(2) Afisa leseni atawasilisha nakala ya kibali cha uwindaji wa wenyeji kwa Kamishna Mhifadhi kilichotolewa katika mamlaka yake baada ya kumalizika kwa msimu husika wa uwindaji.

(3) Kamishna Mhifadhi-

(a) hatapeleka mgao wa mapato unaotokana na wanyamapori waliowindwa;

(b) hatatoa mgao wa wanyamapori watakaowindwa,

kwa wilaya ambayo itakiuka masharti ya kanuni hii.

Uuzaji wa nyamapori

14. Mwindaji mwenyeji yeyote ambaye anahitaji kuuza nyamapori ambayo ameipata kutokana na uwindaji wa wenyeji atalazimika kufuata masharti yaliyowekwa katika sheria nyingine yoyote inayosimamia uuzaji wa nyamapori.

Mwindaji mwenyeji kubeba kitambulisho

15.-(1) Kila Mwindaji mwenyeji atatakiwa kubeba kitambulisho cha mwindaji mwenyeji wakati wote wa safari ya uwindaji.

(2) Mtu yeyote ambaye anakiuka kanuni ndogo ya (1) atakuwa ametenda kosa, na atakapotiwa hatiani atatozwa faini ya shilingi laki tatu au kifungo jela kwa kipindi cha miezi sita au vyote.

(3) Kamishna Mhifadhi anaweza kufifilisha kosa chini

ya kanuni ndogo (1) kwa mujibu wa Sheria kwa kutoza faini ya shilingi laki mbili.

Kupotea kwa kitambulisho

16. Endapo kitambulisho cha mwindaji mwenyeji kimepotea-

(a) atapaswa kutoa taarifa polisi ya upotevu huo; na

(b) atatakiwa kuwasilisha taarifa ya upotevu wa kitambulisho kwa kamanda wa kanda husika kwa ajili ya maombi ya kupatiwa kitambulisho kipya.

Usimamizi wa nyara

17.-(1) Kila mwindaji mwenyeji atahakikisha kuwa-

(a) mnyamapori amechunwa ngozi vizuri pamoja na nyara nyingine zimewekwa chumvi, zimekaushwa na kutunzwa vizuri;

(b) isipokuwa kama atapata cheti cha umiliki wa nyara, atakabidhi ndani ya muda wa siku thelathini, ngozi pamoja na nyara nyingine isipokuwa nyama kwa afisa leseni aliyetoa kibali;

(c) anaambatana na mfuata nyayo ambaye ataongoza katika kufuatilia wanyamapori.

(2) Afisa leseni baada ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Kamishna Mhifadhi ataondosha nyara zilizowindwa kutoka kwa wawindaji wenyeji kwa kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa na Kamishna Mhifadhi.

Uhamishaji wa nyara

18.-(1) Mtu hatahamisha umiliki wa nyara yoyote inayotokana na mnyamapori aliyewindwa kupitia kibali cha uwindaji wa wenyeji kwa mtu asiye raia bila kupata idhini ya Kamishna Mhifadhi.

(2) Bila kuathiri Kanuni ndogo ya (1), iwapo idhini ya uhamishaji imetolewa, mhamishaji atatakiwa kulipa ada ya uhamishaji ambayo ni tofauti kati ya ada ya uwindaji wa kitalii na ada ya uwindaji wa wenyeji kwa mnyamapori husika.

## SEHEMU YA TATU
## MAKOSA NA ADHABU

Adhabu ya jumla

19. Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti ya Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa, na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo cha muda usiopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote.

## SEHEMU YA NNE
## MASUALA MENGINEYO

Miongozo

20. Kamishna Mhifadhi anaweza kutoa miongozo kuhusiana na-
(a) mtihani wa wawindaji wenyeji;
(b) kuainisha mfumo wa ugawanyaji wa faida za kiuchumi zinazotokana na uwindaji wa wenyeji kwa ustawi wa jamii;
(c) uwindaji katika maeneo yenye rasilimali ya wanyamapori;
(d) kusajili, kurejesha, kuchakata nyara na kuondosha; na
(e) utekelezaji wenye ufanisi wa Kanuni hizi.

Rufaa

21.-(1) Mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamishna Mhifadhi, ndani ya siku thelathini baada ya kupokea uamuzi huo, anaweza kukata rufaa kwa Waziri.

(2) Waziri, baada ya kupokea rufaa iliyowasilishwa kwake atatoa uamuzi kuhusu rufaa husika ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kuwasilisha kwa rufaa hiyo.

(3) Mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Waziri anaweza kutafuta shufaa Mahakama Kuu.

Kufuta
TS. Na.
383 la Mwaka
2021

22.-(1) Kanuni za Uwindaji wa Wenyeji za Mwaka 2021 zimefutwa.

(2) Masharti ya Kanuni hizi hayataathiri kampuni za uwindaji wa wenyeji ambazo zilipatiwa maeneo kwa ajili ya shughuli za uwindaji wa wenyeji kupitia Kanuni za Uwindaji wa Wenyeji za Mwaka 2021 kama zilivyofutwa zitaendelea kutumika kwa kusimamia shughuli za uwindaji kwa makampuni husika mpaka pale mikataba yao itakapoisha muda wake.

**JEDWALI LA KWANZA**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6)*

**FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA UWINDAJI**

Weka picha

1. Jina kamili la mwombaji: ...........................................................................................
2. Jinsi :...........................3. Umri :........................4. Uraia:……………..……………..
5. Anwani ya Makazi ...........................................................................................
6. Ikiwa ni mgeni Mkazi: (a) Pasipoti Na: .........................................................
(b) Tarehe ya toleo la Visa:……………………………..………
(c) Tarehe ya kumalizika kwa muda: ..........................
(d) Kibali cha kazi Na: ………………………………………………
(e) Tarehe ya toleo :...................................................
(f) Tarehe ya kumalizika kwa muda ...........................

7. Silaha: (a) Aina: ...........................................................................................
(b) Ukubwa wa risasi:………………………………(c) Namba ya Silaha: ……………………………
(d) Namba ya Kadi ya Silaha :………………………(e) Imetolewa tarehe: …………………………..
(f) Namba ya Leseni ya umiliki wa Silaha………… (g) Tarehe ya kuisha matumizi …………………
(h) Kipenyo cha risasi……………….…………….

8. Kadi ya mwindaji
(a) (i) Namba ya kadi: ...................................... (ii) Mahali ilipotolewa: ...................................
(b) Tarehe ya kutolewa :………………….……………

9. Taarifa kama ulishawahi kukutwa na hatia ya kosa la jinai chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ..........................................................................................................................................................................................................................................................................................................................

10. Taarifa za kukataliwa / kufungiwa/ kufutwa kwa leseni yoyote uliowahi kuomba/ kupewa na mamlaka nyingine za usimamizi Tanzania ...........................................................................................................................

..........................................................................................................................
.......................................................

11. (i) Toa maelezo ya Wanyamapori wanaohitajika;

| Na: | Kifurushi cha uwindaji | Aina ya Mnyamapori | Idadi ya wanyama | Ada ya Mnyama | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

(ii)Taarifa za wageni watazamaji

| Na: | Jina | Umri | Utaifa | Namba ya Kitabulisho cha Taifa/ Hati ya kusafiria | Idadi ya Siku | Date | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Tangu | Mpaka |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |

(iii) Taarifa za kundi la Wawindaji.

| Na: | Jina | Umri | Namba ya Kitabulisho cha Taifa/ Hati ya kusafiria | Idadi ya Siku | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

(iv)Magari.

| Na: | Aina ya gari | Namba ya usajili |
|---|---|---|
| | | |
| | | |

Angalizo: (i) Mwindaji mwenyeji anaruhusiwa kutumia magari matatu (4WD) tu kwa kila kibali baada ya kulipa ada zinazohusika.
(ii) Kila gari la ziada litalipiwa ada mara mbili ya ada ya kawaida iliyoainishwa.

12.Eneo ambalo uwindaji utafanyika
……………...........................................................................................

13.TAMKO LA MWOMBAJI.

Ninatamka kwamba maelezo yaliyotolewahapo juu ni ya kweli na ninaelewa masharti ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, na sheria ndogo zilizotungwa chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.

........................................... 20………….
Mahali .................................................
......................................................
Saini ya Mwombaji

ANGALIZO:
(1)Maombi haya yataambatishwa na kibali iliyomalizamuda wake.
(2) Taarifa zisizo sahihi zitapelekea kuchukuliwa kwa hatua za kijinai.

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(2))*

KIBALI CHA UWINDAJI WA WENYEJI

Namba: ……

*HAIAMASHWI*

| | |
|---|---|
| 1. | Kituo…………………….………………. |
| 2 | Tarehe ya kutolewa……………………………….. |
| 3 | Tarehe ya kumalizika……………………………… |
| 4 | Imetolewa kwa ………………………………………….. |
| 5 | Kwa anuani…………………………………………. |
| 6 | Mmiliki wa kitambulisho Na……………………. |
| 7 | Mahali kilipotolewa…………………….. |
| 8 | Tarehe……………………………. |
| 9 | Imeidhinishwa kuwinda kwa kutumia………………………..Toleo Na …………………… |
| 10 | Imesajiliwa kwa Kadi Na ……………………ya Tarehe…………………… |
| 11 | imeidhinishwa kuwinda wanyama waliotajwa hapo chini. |

(i) Orodha ya wanyama waliotolewa

| NA | Kifurushi cha uwindaji | Aina ya wanyama | Kiasi | Ada(Tzs) | Maoni (Kwa matumizi ya ofisi) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |

(ii) Orodha ya wageni watazamaji

| NA | Jina | Umri | Utaifa | Kitambulisho cha Taifa /Hati ya kusafiria | Idadi ya siku | Tarehe | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | kutoka | kwenda |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |

(iii) Orodha ya kundi la wawindaji

| NA | Jina | Umri | Kitambulisho cha Taifa /Hati ya kusafiria | Maoni (Kwa matumizi ya ofisi) |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |

(iv) Magari

| NA | Aina ya Gari | Nambari ya Usajili |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |

ANGALIZO: (i) Kila mwindaji mwenyeji ataruhusiwa kutumia magari matatu tu yenye 4WD kwa kibali baada ya kulipa Ada zilizoainishwa.
(ii) Gari lolote litakaloongezwa litalazimika kulipa mara mbili ya Ada iliyoainishwa

Kiasi cha Fedha kilichopokelewa Tshs ( Kwa maneno…………………………………………………………………………....)
(Tshs ……………………………….…………….) ikiwa ni malipo ya jumla ya mujibu wa Sheria.
Stakabadhi ya malipo
Na………………………………………..Tarehe……………
…………………………
………………………………………………………………
……………………………..

……… …………………………………..
Saini ya Afisa aliyetoa kibali na Mhuri wa Ofisi

………………………
Saini ya Mmiliki

REJISTA YA WANYAMA WALIOUWAWA NA MAJERUHI

| Na. | Aina ya Wanyama | Jinsia | Umri | Usajili | Hati ya Usajili wa Nyara | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Na | Tarehe | Mahali ilipotolewa |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |

<u>TAMKO</u>

Mimi …………………………………………………………..natamka kuwa taarifa zilizopo hapo juu ni za kweli kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 61(1) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, kuwa wanyama wote waliowauwa tangu kuanza kutumika kwa kibali hiki.
Anuani………………………………..
Tarehe ……………………..20………..

………………………
…………………………………………………..
Saini ya MmilikiSaini ya Afisa ambaye kibali kinarudishwa kwake

<u>ANGALIZO:</u>(1) Wanyama wote waliowindwa au kujeruhiwa watawekwa kwenye kumbukumbu na nyara za wanyama waliouwawa zitasajiliwa na kukabidhiwa kwa afisa leseni.

(2) Kibali kitakabidhiwa kwa afisa lesseni ndani ya siku 30 tangu kumalizika au kabla ya mmiliki kuondoka eneo lilotolewa kibali

______________

JEDWAL LA TATU

______________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1))*

ADA ZA WANYAMAPORI WANAOWINDWA KATIKA UWINDAJI WA WENYEJI

A. WANYAMA

| Na: | Jina la Mnyamapori | Ada ya Mnyamapori (Tsh) | |
|---|---|---|---|
| | | Mkazi | Mgeni Mkazi |
| 1 | Nyati | 200,000 | 400,000 |
| 2 | Pongo | 80,000 | 160,000 |
| 3 | Nguruwe-Mwitu | 80,000 | 160,000 |
| 4 | Digidigi (sunguya) | 60,000 | 120,000 |
| 5 | Nsya | 40,000 | 80,000 |
| 6 | Pofu (Mbunju) dume | 300,000 | 600,000 |
| 7 | Swala (Granti) dume | 80,000 | 160,000 |
| 8 | Swala Tomi Dume | 50,000 | 100,000 |
| 9 | Sungura | 10,000 | 20,000 |
| 10 | Kongoni/Konzi | 100,000 | 200,000 |
| 11 | Swalapaladume | 80,000 | 160,000 |
| 12 | Ngiri/Mbango | 50,000 | 100,000 |
| 13 | Tohe – ndupe –dume | 100,000 | 200,000 |
| 14 | Tohe – kusidume | 100,000 | 200,000 |
| 15 | Nyamera | 100,000 | 200,000 |
| 16 | Nyumbu | 100,00 | 200,000 |
| 17 | Pimbi | 10,000 | 20,000 |
| 18 | Pundamilia | 300,000 | 600,000 |

B. NDEGE

| Na | Jina la Ndege | Ada ya Ndege (Tsh) | |
|---|---|---|---|
| | | Mkazi | Mgeni mkazi |
| 1 | Mabata | 20,000 | 40,000 |
| 2 | Sululu | 5,000 | 10,000 |
| 3 | Firigogo | 5,000 | 10,000 |
| 4 | Njiwa | 5,000 | 10,000 |
| 5 | Kanga | 15,000 | 30,000 |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2))*

KITAMBULISHO CHA MWINDAJI WA WENYEJI

Namba: …………

**Weka Picha**

HAKIHAMASHWI

1. Jina; ………………..……………………………………………………………………………
2. Anuani; ………………………………………………………………………………………………
3. Tarehe ya kutolewa ;…………………………..…Tarehe ya kumalizika; …………… ………
4 Nambari ya Kitambulisho; ………………………………………………………………………
5 Sehemu ilipotolewa; ………………………………………………………………………………

___________ __________________________

Saini ya Mmiliki Saini ya Kamanda Mhifadhi na Muhuri

ANGALIZO:

(1) Kitambulisho cha Mwindaji mwenyeji kinapaswa kubebwa kipindi cha uwindaji.
(2) Kitambulisho cha Mwindaji mwenyeji kitatumika kwa miaka miwili.
(3) Kitambulisho ni mali ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kama kikipotea toa taarifa TAWA.

S. L.P. 2658 MOROGORO
SIMU;+255(0)232934204

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(2) na 10(5))*

**(A)** ADA ZA UWINDAJI WA WENYEJI

| Ada( Mtu / Gari) kwa Siku | Raia (TZS) | Mgeni (TZS) |
|---|---|---|
| Ada ya Uhifadhi | 5,000 | 10,000 |
| Ada ya Mgeni Mtazamaji | 10,000 | 20,000 |
| Ada ya Gari | 15,000 | 30,000 |

**(B)** Ada ya Kitambulisho cha Mwindaji mwenyeji itakuwa TZS 30,000/=

Dodoma,
24 Oktoba, 2022

PINDI H. CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*